**CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHA NGOME**

**(NGOMESACCOS LTD)**

**DSR 991**

# SERA YA USALAMA,MAZINGIRA NA MAJANGA

**TOLEO LA 1: 2020**

**CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHA NGOME**

**(NGOMESACCOS LTD)**

**DSR 991**

# SERA YA USALAMA,MAZINGIRA NA MAJANGA

**TOLEO LA 1: 2020**

## SERA YA USALAMA NA MAZINGIRANGOMESACCOS LTD

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 HISTORIA YA CHAMA

NGOMESACCOS LTD yenye nambari ya usajiri DSR 991 ilisajiliwa tarehe 30 April 2007, chini ya sheria ya Ushirika No. 20 ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2004, kama inavyorejewa na sheria ya sasa ya Ushirika No. 6 ya mwaka 2013 na kanuni zake . Wanachama wa NgomeSACCOS Ltd wanatokana na fungamanisho (common Bond) ya Maafisa ,Maaskari , Wastaafu pamoja na Watumishi wa Umma wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na wale waliohamia wizara nyingine wakiwa wanachama Hai wa Ngome SACCOS.

### UTANGULIZI

1. Sera ya mazingira na usalama imetayarishwa ili kukidhi matakwa ya NEMC Tanzania, inayo agiza kwamba kabla ya kampuni au asasi yoyote kuanzishwa huduma mahali eneo lakazi mazingira lazima yapewe kipaumbele kwa mustakabali wa wafanyakazi, majirani na wateja wanaofika ofisini kwaajiri ya huduma.
2. NGOMESACCOS LTD ilifungua ofisi zake Mwenge mwezi Desemba 2009, baada ya kuhama kutoka Makao Makuu ya Jeshi. Aidha kabla ya kufungua ofisi za Ngome SACCOS LTD jengo lililopo NGOMESACCOS LTD lilikuwa linamilikiwa na band coy.
3. Sera ya mazingira na usalama imetungwa ili kufanikisha yafuatayo:
   a. Utunzaji na uboreshaji wamazingira katika eneo la kazi kudumisha usalama ndani na nje ya jengo la NGOMESACCOS LTD.
   b. Kuweka mazingira safi ili kuepuka wanyama wakali na wadudu.
   c. Kuhakikisha kwamba usafi wa eneo la ndani na nje ya jengo la NGOMESACCOS LTD unadumishwa.

e. Kuhakikisha kwamba chama kinaboresha mazingira ya eneo la kantini ili kupambana na magonjwa mbalimbali yanayo sababishwa na uchafu.

## SEHEMU YA PILI

### USALAMA

Usalama eneo la kazi ni mhimu ili chama kiweze kufikia malengo yake kuwa chama cha akiba na mikopo bora Tanzania.

Aidha mambo ya usalama yanahusisha usalama wa Watu, nyaraka, fedha, na jengo la chama kwa ujumla.

a. Usalama wa nyaraka utahusisha uboreshaji wa utunzaji wa nyaraka laini "**soft copy**" kwenye mfumo wa TEHAMA na sehemu za kuhifadhia nyaraka zilizo chapishwa kwenye makaratasi **"hard copy".**
b. Usalama wa fedha utahusisha uimarishaji wa chumba cha kuhifadhi fedha **"strong room"** na ulinzi eneo lote la jengo la chama kwa kutumia walinzi wajeshi toka kikosi cha karibu.
c. Usalama wa watu kazini ni muhimu kutokana na madhara yanayoweza kusababishwa na wizi kwa kutumia silaha, ugaidi, na mambo ya kijasusi kwa lengo la kupata taarifa za chama kwa nia ovu.
d. Kuwepo kisanduku cha huduma ya kwanza (First Aid Kit) sehemu ya wafanyakazi na wateja.
e. Kuwepo na utaratibu wa wateja na watendaji kufanyiwa upekuzi (vetting) ili kuepuka madhara ya ugaidi na vitendo vingine ovu wanapoingia kwenye jengo.
f. Usalama wa jengo unahusisha uimarishaji wa jengo kwa kufanya ukarabati kwa maeneo yote yanayo hitajika kufanyiwa ukarabati ili kuepusha jengo kubomoka au kuezuliwa na mvua inayo ambatana na upepo mkali **kimbunga**.

g. Usalama wa jengo katika kukabiliana na radi wakati wa mvua kushirikisha wataalam wa ujenzi na majanga ya radi ili kufunga mfumo wa kupambana na majanga ya radi "thunder arrester system".
h. Usalama wa chama utahusisha utoaji wa elimu ya usalama katika maeneo yote ya kazi tangu wakati wa mapokezi ya wateja, nyaraka,fedha, utunzaji wa nyaraka husika na fedha katika kasiki.
i. Usalama wa fedha wakati wa kupeleka na kuchukua ili malipo ya weze kufanyika kwa walengwa lazima uwe mzuri.

## SEHEMU YA TATU
## TAHADHARI DHIDI YA MAJANGA MAJANGA

Majanga ni matukio yanayoweza kutokea na kusababisha maafa na uharibifu wa mali katika kampuni au taasisi yeyote ile. Hata hivyo majanga yapo ya asili kama vile tetemeko la ardhi, kimbunga na radi. Aidha, kuna majanga ambayo siyo ya asili yanasababishwa na shughuli za kawaida katika utendaji wa kila siku kama majanga ya moto. Hatua za tahadhari zinazo paswa kuchukuliwa dhidi ya majanga husika ni kama ifuatavyo:

a. Majanga ya asili kama radi, upepo mkali kimbunga, na tetemeko la ardhi.

(i) Kuwe na eneo mbadala kwa ajiri ya kuokolea mali na waathirika wa majanga.
(ii) Kuwe na vifaa maalumu vya kusaidia kazi ya kuokoa wahanga wa majanga kama vifaa vya huduma ya kwanza
(iii) Kuwe na gari la kubebea wagonjwa (ambulance)
(iv) Chama kiwe na mtu anayehusika na mambo ya dharula linapotokea janga la umeme.
(v) Paa la jengo lazima liwe imara ili kuhimili misukosuko ya mvua ya kimbunga.
(vi) Kuwe na ngazi kubwa ya kushuka chini kutoka juuya jengo.

b. Kwa majanga yanayotokana na shughuli za kawaida kazini kama moto vifaa vifuatayo lazima viwepo:
   (i) Kifaa cha kuzimia moto wa kawaida kama **"carbon dioxide fire extinguisher"**
   (ii) Kifaa cha kuzimia moto wa mafuta **"foam fire extinguishers"**
   (iii) Kifaa cha uzimaji moto chenye kutumia poda **"Chemical powder fire extinguisher"**
   (iv) Kifaa cha uzimaji moto cha kutumia maji " **wet fire extinguisher"**
   (v) Kuwe na mablanket ya kuzimia moto yasiyopungua sita(6) **"fire proof blanket"**
   (vi) Kuwe na mfumo wa maji kwa ajili ya kuzima moto **"fire hydrant System".**

c. Kufunga vifaa vya moto vinavyo weza kufanya kazi kabla ya janga la moto kutokea kama vile
   (i) Smoke detector system
   (ii) Fire waterise system
   (iii) Heat detector system
   (iv) Flame detector system
   (v) Gas detector system`
   (vi) Automatic sprinkler system
   (vii) Alarm system

d. Kufanya mafunzo na mazoezi ya kukabiliana moto na majanga kabla ya kutokea:
   (i) Namna ya kutumia vifaa vya kuzima moto
   (ii) Kuokoa wahanga wa majanga na mali
   (iii) Kutoa taarifa ya maafa na majeruhi ya wahanga kwa mamlaka husika.
   (iv) Kutoa huduma ndogo baada ya majanga kwa waliojeruhiwa na kuwapeleka hospitali kwa uchunguzi na matibabu zaidi.

(v) Kufanya ukaguzi wa vifaa vya kuzimia moto mara kwa mara

(vi) Kupata mafunzo,semina za kukabiliana na majanga ya moto mara kwa mara.

(vii) Kufanya mazoezi ya kuzima moto kwa kushitukiza angalau mara mbili kwa mwaka, ili watendaji wawe na uelewa mkubwa wa nini cha kufanya pindi majanga ya moto yanapotokea.

(viii) Kuonesha mlango wa dharula (exit door) ili kurahisisha uokoaji wakati wa majanga.

(ix) Kuonesha sehemu ya makutano (fire assembly area) kukiwa kumetokea janga la moto.

**<u>SEHEMU YA NNE</u>**

## TAHADHARI DHIDI YA MAJANGA YANAYOTOKANA NA TETEMEKO LA ARDHI

Tetemeko la ardhi ni mtikisiko wa ardhi unaotokana na nguvu za kiasili/jiografia au shughuli za kibinadamu. Tetemeko linaweza kuepukika kwa kuwa na vifaa vifuatavyo .

(i) Kamba maalum zenye urefu usiopungua mita 100 (manila)

(ii) Kifaa maalum (clipping kalabina) kinachofanya kazi pamoja na kamba maalum wakati wa kuokoa wahanga kwenye majengo marefu.

(iii) Kupata mafunzo ya kuparamia na kushuka kwa kamba majengo marefu kwa kutumia vifaa vilivyotajwa.

(iv) Kuwa na ngazi maalum na magodoro ya "sponch" kwa kazi ya kuokolea.

(v) Kufanya mipango ya huduma ya kwanza na kupeleka wa hanga hospitali kwa uchunguzi na matibabu zaidi.

(vi) Kuwa na vifaa vya kutoa tahadhari wakati wa majanga.

**a. Mambo ya kuzingatia ili kukabiliana na majanga ya kimbunga, radi na mafuriko katika eneo la kazi.**

(i) Kukabiliana na kimbunga majengo ya ofisi yanapaswa kuimarishwa sehemu za paa .Ni vyema majengoyafanyiwe ukaguzi mara kwa mara ili kuona kama majengo yapo imara kukabiliana na kimbunga.

(ii) Kununua maboya ya kujazwa upepo yanayo weza kuelea kwa ajiri ya kuokoa watu wakati mafuriko yanapo kuwa jirani na majengo ya ofisi.

(iii) Ili kukabiliana na majanga ya radi majengo yafungwe kifaa maalum vya kunasa moto wa umeme wa radi "**thunder arrester**".

**b. UTUNZAJI WA TAKWIMU MUHIMU"DATA" DHIDI YA MAJANGA**

Mambo muhimu ya kuzingatia kwa ajili ya Utunzaji wa takwimu za ofisi dhidi ya majanga ni kama ifuatavyo:

a. Takwimu zitunzwe kwenye "soft copy", "hard copy", na "external hard disc".
b. Aidha utunzaji unaweza kufanyika hata nje ya ofisi za NGOMESACCOS LTD ili ikitokea upotevu wa takwimu kutokana na majanga iwe rahisi kuzipata tena.
c. Chumba maalumu kijengwe (fire proof custody) kuzuia takwimu, nyaraka na fedha isiwe rahisi kupotea kutokana na majanga.
d. Kuwe na utaratibu wa kufuatilia hali ya hewa na kupanga mipango ya kukabiliana na majanga.
e. Kuwe na eneo maalum kwa ajiri ya kazi ya kuokolea wahanga wa majanga.
f. Mkuu wa kikundi cha uokozi atatayarisha mpango wa mafunzo ya uokozi kwa majanga mbali mbali kwa mwaka mzima na kualika wawezeshaji watalaamu katika idara za majanga mbali mbali.

**HITIMISHO.**

Sera hii imeandaliwa na Bodi ya Ngome SACCOS na Kamati ya Usimamizi iliyokasimiwa madaraka kwa niaba ya wanachama kwa barua yenye kumbukumbu Na. MA.82/309/20/14 ya tarehe 05 AGOSTI, 2020 na itaanza kutumika baada ya kuidhinishwa na Mrajis

Mwenyekiti

Katibu

NGOME SAVING AND CREDIT CO-OPERATIVE SOCIETY LIMITED
NGOME SACCOS LTD
REG. DSR 991
P. O. Box 35923
DAR ES SALAAM

TANZANIA
Approved this 01ST
day of MARCH 2021
Asst. Registrar of Cooperative Societies